

Kuelewa na Kuheshimu Hisia za Wengine

KISA CHA 1

Selam alikuwa kwenye mlo wa mchana pamoja na marafiki zake, lakini alipokimbilia msalani aliiacha simu yake mezani. Alipokuwa hayupo, rafiki yake Mwikali aliichukua simu ya Selam na kuanza kuzisoma meseji zake. Ujumbe wa maandishi wa kwanza aliouona ulikuwa ni wa hasira uliotoka kwa mama yake Selam kwa sababu hakufaulu hesabu.



Je, hali hiyo inaweza kumfanya Selam ajisikiaje? _____



Kwa nini Selam asingependa kuwaambia marafiki zake kuhusu matokeo yake mabaya? _____



Je, matendo ya Mwikali yanakubalika? _____



Je, marafiki wengine watajisikiaje kuhusu matendo ya Mwikali wakati wa chakula cha mchana? _____



Una maoni gani kuhusu Mwikali? Je, Mwikali alitenda kwa kuzingatia maadili? Je, ungependa kuwa rafiki yake Mwikali?



Ungejihisi vipi kama mtu angekutendea hivyo? _____



Je, kusoma meseji za wengine ni sawa? Vipi ikiwa una wasiwasi kuhusu rafiki yako? _____

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Facebook na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.

Kuelewa na Kuheshimu Hisia za Wengine

KISA CHA 2

Yonas anaongea na Masese kisha anateleza na kuanguka chini. Masese anafikiri hali hiyo inachekesha sana kisha anampiga picha, lakini Yonas hacheki na anaonekana ameaibika.



Je, kwa nini huenda Masese akachapisha picha hiyo mtandaoni? _____



Je, kwa nini Yonas ameuadhika? _____



Je, unafikiri Yonas anatakiwa amwambie nini Masese? _____



Ungejihisi vipi kama mtu angekupiga picha ya kuaibisha? Je, ungependa iwekwe kwenye mtandao? _____



Je, hali hii ni tukio la uonevu? _____

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Facebook na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.

Kuelewa na Kuheshimu Hisia za Wengine

KISA CHA 3

Victoria ni mwanafunzi mwenye umri wa miaka 15 aliye na ndugu wawili, mama na marafiki wengi anaosoma nao. Victoria na Marek wanasoma wote na wanafanya kazi pamoja kwenye mradi katika darasa la sayansi. Jana, walifanya mtihani wa sayansi na kila mtu alipokea matokeo yake, Marek aligundua kwamba Victoria hakufurahia matokeo hayo. Wiki inayofuata, Victoria hakuja shuleni kwa siku kadhaa, kwa Marek alilazimika kufanya kazi kwenye mradi huo wa sayansi mwenyewe. Aliporudi, Victoria alimwambia Marek kwamba alilazimika kwenda kwa daktari. Hata hivyo, hasemi ni kwa sababu gani.



Je, mtu yeyote anahitaji kujua kuhusu matokeo ya mtihani ya Victoria? Historia yake ya matibabu? Kwa nini?



Je, Victoria angependa kuzungumza na nani kuhusu masuala haya? _____



Katika maisha yako, ni mifano gani ya taarifa ambazo unataka wazazi/walezi wako wazione lakini siyo marafiki zako au kinyume chake?

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Facebook na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.